JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

Mhe. Mstahiki Meya
Baraza la Madiwani la Mwaka,
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA. Tarehe: 10/08/2023

YAH: TAARIFA YA UTENDAJI KAZI NA UWAJIBIKAJI WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA KWA MWAKA 2022/2023

Mheshimiwa Mstahiki Meya, Naomba kuwasilisha taarifa hii kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Manispaa Kifungu Na. 7(3) kifungu kidogo (C). Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imekuwa na mafanikio katika utekelezaji wa shughuli za Serikali katika sekta mbalimbali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mstahiki Meya, Sekta ya Fedha na Biashara: Halmashauri ya Manispaa kwa mwaka 2022/2023 iliidhinishwa kukusanya, kupokea na kutumia shilingi. 67,769,480,428 kwa ajili ya kulipa Mishahara ya watumishi, Matumizi mengineyo na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambapo hadi kufikia Juni 30, 2023 jumla ya shilingi. 72,907,411,629 zimepokelewa sawa na 108%. Kati ya fedha hizo, Bajeti ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri ni shilingi. 13,524,000,000 ambapo hadi kufikia Juni 2023 shilingi. 15,800,740,154 zimekusanywa sawa na 117%. Mafanikio haya kwa sehemu mkubwa yamechangiwa na mradi wa kupanga, kupima na kumilisha katika eneoa la Nyafula Kata ya Sangabuye pamoja na ufuatiliaji wa karibu wa vyanzo vingine.

Sekta ya Biashara na Viwanda: Sekta hii imeendelea kuwa muhimili muhimu wa Uchumi wa Manispaa kwa maana ya wananchi na Halmashauri. Vyanzo vya mapato vinavyotegemea Sekta hii ni pamoja na

Ushuru wa huduma, leseni za biashara, upangaji kwenye masoko, upangaji kwenye nyumba za Halmashauri, ushuru wa shughuli za utamaduni, ushuru wa kupakia na kushusha, ada ya nyumba za kulala wageni, leseni za vileo, ushuru wa mabasi pikipiki/bajaji na daladala. Hadi kufikia Juni 203 vyanzo hivi vyote vimekusanya shilingi 4,843,959,908

Sekta ya Utawala na Rasilimali watu: Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ina Jumla ya watumishi 3,443 wakati mahitaji halisi ni watumishi 4,409 na hivyo bado kuna upungufu wa watumishi 958 hususani katika sekta ya ujenzi, walimu wa sayansi, watalaamu wa sekta ya afya na watendaji wa mitaa.

Aidha, Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya watumishi 31 wamehama kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kwenda katika vituo vingine vya kazi kwa sababu mbalimbali. Watumishi 112 wamehamia katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela wakitokea katika vituo mbalimbali vya kazi ambavyo walikuwepo hapo awali. Watumishi 28 wamestaafu Utumishi wa Umma kwa kwa lazima na kwa hiari kwa mujibu wa Sheria. Jumla ya watumishi 05 walifariki na Halmashauri iligharamia shughuli zote za mazishi kwa watumishi hao kwa mujibu wa kanuni za Utumishi wa Umma

Sekta ya Elimu Msingi: Wilaya ina jumla ya shule 139 za Msingi, kati ya hizo shule 58 ni za Binafsi na shule 81 ni za Serikali. Kuna jumla ya wanafunzi 80,869 wa shule za serikali, kati yao wavulana ni 39,309 na wasichana ni 41,560. Walimu walioajiriwa katika shule za serikali ni walimu 1413 (Me 367 Ke 1046). Aidha, Halmashauri ina vituo kumi (10) vinavyotoa Elimu Maalum kwa wanafunzi wenye Mahitaji Maalum wapatao 460 ambavyo ni Pasiansi, Kirumba, Ibeshi, Buswelu, Kayenze, Sabasaba, Nyasaka, Buzuruga, Nyamhongolo na Nyamanoro. Hali ya ufaulu kwa wanafunzi wa darasa la saba imeongezeka kutoka wanafunzi 10,527 mwaka 2021 sawa na asilimia 94.2 hadi 12,548 mwaka 2022 sawa na asilimia 95. Hadi kufikia Juni 2023, jumla ya shilingi. 3,470,123,847.10 zimetolewa kwa ajili ya Miradi ya Elimu Msingi na Elimu bila Malipo

Sekta ya Elimu ya Sekondari: Wilaya ina shule 56 za Sekondari ambapo kati ya hizo shule 32 ni za Serikali na 24 ni za Binafsi. Kuna jumla ya wanafunzi 33,569 wa shule za Sekondari za Serikali, kati ya wasichana ni 17,364 na wavulana ni 16,205 walimu walioajiriwa katika shule za serikali ni walimu 1093 (Me 617 Ke 476). Hali ya ufaulu wa kidato cha nne imeongezeka kutoka wanafunzi 6,462 kwa mwaka 2021 sawa na asilimia 93 hadi 6,470 mwaka 2022 sawa na asilimia 95.4. Hadi kufikia Juni 2023, jumla ya shilingi. 6,849,827,219.02 zimetolewa kwa ajili ya miradi ya elimu Sekondari na Elimu bila Malipo

Sekta ya Afya: Halmashauri ya Manispaa ina jumla ya vituo 66 vya kutolea huduma za Afya ambapo vya Serikali 23, Taasisi binafsi 4, Mashirika ya dini 3 na watu binafsi 36. Huduma zinazotolewa katika vituo hivi ni huduma za wagonjwa wa nje (OPD), huduma za kulaza (IPD), huduma za Afya ya uzazi (Baba, Mama na Mtoto), ushauri nasaha na kupima na kutoa huduma za afya mashuleni. Katika kuendelea kuboresha huduma za Afya, Manispaa ya Ilemela inaendelea na ukamilishaji wa wodi 3 katika hospitali ya Wilaya. Aidha Katika mwaka 2022/23 jumla ya shilingi. 1,638,379,416.39 zimetolewaa kwa ajili ya shughuli za uboreshaji wa sekta ya Afya na miundombinu yake ambapo zahanati na wodi za akina mama zimeendelea kujengwa na kuboreshwa katika maeneo mbambali.

Program ya Lishe: Katika kipindi cha Mwaka 2022/2023 watoto 2,503 (2.0%) walikuwa na utapiamlo wa kati, watoto 147 (0.1%) walikuwa na utapiamlo mkali, watoto 50 (0.06%) walikuwa na ukondefu. Wazazi na walezi 132,667 (96.6%) wenye watoto chini ya miaka 5 walipata elimu ya ulishaji, watoto 84,149 (111%) umri miezi 6 hadi 59 walipata matone ya vitamin A na dawa za minyoo, wajawazito 75,076 kati ya 83,428 (90%) walipata vidonge vya kuongeza Madini Chuma (FEFO). Shule 140 kati ya 193 sawa na 72.5% zinatoa chakula kwa wanafunzi.

Sekta ya Maendeleo ya Jamii: Halmashauri imehamasisha wananchi katika kujiunga na vikundi vya kiuchumi ambapo ina jumla ya vikundi 1,709 kati ya hivyo vikundi vya wanawake vipo 429, vikundi vya vijana vipo 106 vikundi vya watu wenye ulemavu vipo 08 vya wanaume vipo 44, na vya

watu mchanganyiko vipo 665. Katika mwaka wa fedha 2022/23 Halmashauri imefanikiwa kutoa mikopo yenye jumla shilingi. 479,000,000/= katika vikundi 44 ambapo kati ya fedha hizo shilingi. 274,000,000/= zilitolewa kwa vikundi 32 vya wanawake, shilingi. 201,000,000/= kwa vikundi 10 vya vijana na shilingi. 4,000,000/= zilitolewa kwa vikundi 2 vya watu wenye ulemavu.

Sekta ya mazingira na udhibiti wa taka ngumu: Jumla ya tani 679 zinazalishwa na wakazi katika Wilaya ya Ilemela kwa siku, kati ya hizo tani 492 sawa na 70.5% zinazalishwa kutoka kwenye kata za mjini (CBD) wakati uwezo wa Wilaya wa kuzoa na kutupa taka kwa kata za mjini ni tani 344 sawa na asilimia 69.9%, uwezo huu unatokana na Wilaya kuwa na gari 1 kusafirisha taka ngumu kwenda dampo. Halmashauri imefanikiwa kununua Mabirika mengine 6. Hadi kufikia Juni 2023, jumla ya Sh. 576,271,068.57 zimetolewa katika sekta hii.

Sekta ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika:
Shughuli zilizofanyika katika kipindi cha mwaka 2022/2023 ni kutolewa kwa elimu ya kilimo bora kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo (Matumizi ya Viuatilifu na Mbolea), Usimamizi na ufuatiliaji wa bei za vyakula vilivyoingia sokoni. Kufuatilia bei na upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo Madukani na uratibu wa maonesho ya Nanenane.

Sekta ya Mifugo na Uvuvi: Kwa mwaka 2022/2023, Halmashauri imefanikiwa kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwemo kufanya mafunzo ya ufugaji na uhamasishaji wa wanyama wadogo Kuku, Sungura na Samaki yamefanyika. Wataalamu wa mifugo walifanya ukaguzi kwenye maduka ya vyakula vya mifugo katika eneo la Manispaa. Sekta ya imeendelea kuchangia uchumi wa Manispaa ambapo hadi kufika Juni 2023 jumla ya Shilingi 1,383,589,302 zilikusanywa kati ya Shilingi 1,426,000,000 sawa na 97%

Sekta ya Mipangomiji: katika kipindi cha 2022/2023 Halmasahauri katika sekta ya ardhi ilifanikiwa kutekeleza mradi wa kupanga, kupima na kumilikisha ambapo ilipata mkopo wa Shilingi 3,589,774,000 kutoka

Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Jumla ya viwanja 3,254 vilipimwa. Mauzo yaliyopatikana kutokana na uuzaji wa viwanja hadi kufikia Juni, 2023 ni shilingi 6,843,358,433.08. Halmashauri imefanikiwa kurejesha fedha zote za mkopo yaani shilingi 3,589,774,000 Wizarani.

Aidha, viwanja ambavyo havijauzwa mpaka sasa ni 162 vyenye thamani ya Shilingi 1,169,942,957.40 na fedha zinazodaiwa kwa waliochukua viwanja na hawajakamilisha ni Shilingi 8,927,844,275.6

Sekta ya Barabara: Manispaa ya Ilemela ina mtandao wa barabara zenye urefu wa Km 870.22 kati ya hizo Kilometa 38.5 ni za kiwango cha lami, Kilometa 2.074 ni barabara za zege, Kilometa 3.74 ni barabara za mawe, Kilometa 89.09 ni changarawe na Kilometa 742.46 ni barabara za udongo. Barabara zinaendelea kuboreshwa kupitia mapato ya ndani kwa kushirikiana na TARURA ambapo kwa mwaka 2022/23 Halmashauri iliingia mikataba ya ujenzi wa barabara Igombe Ziwani kwa kiwango cha zege 0.14km, Barabara ya lami kutoka Hospitali ya Wilaya kuelekea Ilalila 1.3km, matengezo ya stendi ya daladala katika stendi kuu ya mabasi ya Nyamhongolo na matengenezo ya barabara za Msolopa Kangaye kata ya Mecco, Maduka tisa kata ya Ibungilo na Nyasaka, na Nyambiti kata ya Buzuruga. Miradi hii itatumia jumla ya Shilingi 1,675,214,383.93 kupitia mapato ya ndani 2023/24.

Aidha Mhe. Mbunge wa Jimbo la Ilemela Dkt. Angelina Lubala Mabula, kwa fedha za mfuko wa Jimbo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 amewezesha ukarabati wa barabara za mitaa ambapo barabara zilizotengenezwa ni Buyombe – Zahanati ya Lukobe Kata ya Kahama, Barabara ya Zahanati ya Mihama Kata ya Kitangiri, barabara ya Kabuhoro – Kamachumu Kata ya Kirumba, barabara ya Nyasaka – Buswelu, barabara ya Bwiru Stand – Mnarani Sekondari Kata ya Pasiansi, na barabara ya Nyamwilekelwa Kata ya Mecco.

Utekelezaji wa Programu ya TACTIC: Katika mwaka 2022/23 Manispaa ya Ilemela ilifanikiwa kutangaza zabuni za miradi ya ujenzi wa barabara ya Lami ya Busweru-Nyamadoke-Nyamhongolo 9.5 km na barabara ya Busweru-Busenga-Cocacola 3.3km ambapo zipo hatua za mwisho za

kuanza kutekeleza Mikataba. Aidha katika program hii itahusisha pia ujenzi wa soko la Kirumba na barabara za kuzunguka Soko 2.9 km ambapo zipo hatua ya manunuzi

Programu ya 'Green and Smart Cities': Kwa mwaka 2022/23, Manispaa imeendelea na uratibu wa miradi ya uboreshaji miji 'Green and Smart Cities' ambapo upembuzi wa awali (Pre-feasibility study) umefanyika kwa mradi wa ujenzi wa soko la Busweru, Uboreshajiwa soko la Samaki Mwaloni Kirumba, uboreshaji wa Mwalo wa Old-Igombe, uboreshaji wa mwalo wa New-Igombe na uboreshaji wa usafiri Mjini (Urban Mobility).

Sekta ya Misitu: Manispaa imeendeleza program za upandaji miti na utunzaji wa mazingira katika maeneo yote ya taasisi za umma, binafsi na maeneo mengine ya wananchi. Kwa mwaka 2023 Manispaa ya Ilemela imesimamia na kuratibu shughuli za upanadaji miti ambapo imepanda jumla ya miti 336,195 katika maeneo ya shule za Msingi na Sekondari, Zahanati, Vituo vya afya, Hospitali ya Wilaya na meeneo mengine. Miti iliyopandwa inaendelea kutunzwa vizuri. Aidha, Manispaa ina hifadhi 7 za misitu ya asili zijulikanazo kwa jina la Ngitiri ambazo ni Ilekako, Kasamwa, Nyakato, Igalagala, NIMR, Kawekamo na Bwiru. Hifadhi hizi zilianzishwa kwa lengo la kulinda na kuhifadhi mazingira na pia ni makazi ya viumbe hai.

Utekelezaji wa miradi ya Maendeleo: Hadi kufikia Juni 30, 2023 Halmashauri ilikuwa imepokea kiasi cha Shilingi 21,526,062,194.91 kutoka Serikali Kuu, Wadau, Program na Mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Maendeleo kwa mchanganuo ufuatao: -

i. Shilingi 2,200,000,000.00 fedha za Mfuko wa Mhe. Rais kwa ajili madarasa 110 katika shule za sekondari
ii. Shilingi 1,000,000,000.00 fedha za msaada wa kibajeti kupitia Program ya Green and Smart Cities
iii. Shilingi 1,574,900,000.00 fedha za programu ya BOOST kwa ajili ya shule mpya 2 za msingi, madarasa na vyoo.
iv. Shilingi 684,280028.00 fedha za SEQUIP kwa ajili ya shule mpya 1 ya Sekondari, Madarasa na vyoo

v. Shilingi 215,500,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa Bweni, madarasa 3 na vyoo matundu 5 Bwiru Wasichana

vi. Shilingi 300,000,000.00 kwa ajili ya Ununuzi wa vifaa tiba

vii. Shilingi 150,000,000.00 fedha za EP4R kwa ajili ya Ujenzi wa nyumba 2 za 2 in 1 katika shule za msingi na maabara 1 katika shule ya sekondari

viii. Shilingi 4,071,074,280.10 kwa ajili ya Elimu Bila Malipo (EBM) kwa shule za Msingi na Sekondari

ix. Shilingi 140,000,000.00 kwa ajili ya maabara 4 na bweni 1 shule za sekondari

x. Shilingi 155,824,000.00 fedha za Program ya LANES kwa ajili ya bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalumu na madarasa 2 ya mfano ya awali shule ya msingi.

xi. Shilingi 1,150,805,301.76 fedha TASAF kwa ajili miradi na kaya masikini.

xii. Shilingi 83,761,000.00 kwa ajili Mfuko wa jimbo

xiii. Shilingi 578,859,948.62 kwa ajili afua za Afya kupitia mfuko wa pamoja wa Afya, UNICEF, GAVI, Global fund, JHPIEGO, Lishe na ICAP

xiv. Shilingi 8,701,062,636.43.00 zimetolewa kutoka Mapato ya ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi mbali ya Afya, Elimu, uvuzi, upimaji wa ardhi, maendeleo ya jamii, barabara, masoko na biashara

Taarifa ya Miradi imeambatanishwa

Hitimisho

Mheshimiwa Mstahiki Meya, Napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani za dhati kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia fedha za Miradi na za bajeti kwa ujumla, pili shukrani kwa Mhe. Mbunge wa Jimbo la Ilemela Mhe. Dkt. Angeline S.L Mabula (MNEC) kwa kazi kubwa anayofanya katika kuleta maendeleo Jimboni, tatu shukrani kwa Baraza la Madiwani kwa ushirikiano wanaotoa katika kuisimamia Halmashauri. Pia nawashukuru kwa namna ya kipekee kabisa wananchi wote wa manispaa ya Ilemela kwa kuendelea kushirikiana na Serikali kikamilifu katika kuleta maendeleo.

Naomba kuwasilisha,

Adv. Kibamba Kiomoni Kiburwa
MKURUGENZI WA MANISPAA
ILEMELA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MIRADI NA UTEKELEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 JULAI HADI JUNI 2023

NA	CHANZO CHA FEDHA	JINA LA KATA	MIRADI	KIASI TOLEWA	KIASI KILICHOTUMIKA	BAKAA	SEKTA	HATUA YA UTEKELEZAJI
	MAKAO MAKUU							
	Own Source	HQ	Kuwezesha umaliziaji wa Jengo la Utawala	516,596,740.00	516,596,740.00	-	Utawala	Mradi upo katika hatua za umaliziaji
	Own Source	HQ	Malipo ya usajili wa pikipiki moja	37,000.00	37,000.00	-	Utawala	Pikipiki imesajiliwa
	Own Source	HQ	Kuwezesha Ununuzi wa Vishkwambi 52	46,800,000.00	46,800,000.00	-	Utawala	Mradi umekamilika
	Own Source	HQ	Kuwezesha ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo	23,922,000.00	23,922,000.00	-	Mipango na Uratibu	Ufuatiliaji umefanyika
	Own Source	HQ	Kuwezesha shughuli za maandalizi ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024	38,511,400.00	38,511,400.00	-	Mipango na Uratibu	Shughuli zimefanyika
	Own Source	HQ	Kuwezesha mradi wa matofali	268,757,502.00	268,757,502.00	-	Biashara, Viwanda na Uwekezaji	Mradi unaendelea
	Own Source	HQ	Kuwezesha ukarabari wa eneo la Stendi ya daladala Nyamhongolo na Buzuruga	35,453,080.00	35,453,080.00	-	Biashara, Viwanda na Uwekezaji	Mradi umekamilika

	Own Source	HQ	Kuwezesha malipo ya Bili ya maji Nyamhongolo Bus Terminal	9,179,628.00	9,179,628.00	-	Biashara, Viwanda na Uwekezaji	Bill imelipwa
	Own Source	HQ	Kuwezesha ununuzi wa madawati kwaajili ya shule za msingi	34,406,328.00	34,406,328.00	-	Elimu Msingi	Ununuzi umekamilika na madawati yamesambazwa mashuleni
	Own Source	HQ	Kuwezesha Ununuzi wa roller Idara ya Fedha	43,050,000.00	43,050,000.00	-	Fedha	Roller Zimenunuliwa
	Own Source	HQ	Kuwezesha mfuko wa wanawake , vijana na walemavu	597,185,262.59	597,185,262.59	-	Maendeleo ya Jamii	Mikopo inaendelea kutolewa
	Own Source	HQ	Kuwezesha malipo ya Fidia ya ardhi na ulipaji wa sehemu ya deni la ardhi	5,899,780,887.00	5,899,780,887.00	-	Ardhi	Fedha zimelipwa
	Own Source	HQ	Kuwezesha ununuzi wa Computer Desktop pc 1 na Scanner Flatbed pc 1 kwaajili ya Ofisi ya Mkurugenzi	3,737,680.00	3,737,680.00	-	Tehama	Vifaa vimenunuliwa
	Own Source	HQ	Kuwezesha Manunuzi ya UPS(Uninterruptible Power Supply) kwa ajili ya vifaa vya Tehama	6,300,000.00	6,300,000.00	-	Tehama	Vifaa vimenunuliwa

	Own Source	HQ	Kuwezesha ununuzi wa miche ya miti ya matunda kwa ajili ya kusambaza kwenye vituo vya afya	3,475,000.00	3,475,000.00	-	Maliasili	Miche imenunuliwa
	Own Source	HQ	Kuwezesha uzoaji wa taka ngumu	576,271,068.57	576,271,068.57	-	Usafishaji na mazingira	Taka zimezolewa
	Own Source	HQ	Kuwezesha uwekaji wa mtandao wa maji katika kituo cha magonjwa ya mlipuko Buswelu	3,487,648.00	3,487,648.00	-	Afya	Maji yamewekwa
	SERIKALI KUU (Vifaa Tiba)	HQ	Kuwezesha ununuzi wa Vifaa Tiba Hospitali ya Wilaya, kayenze, Nyamadoke disp na Masemele disp	300,000,000.00	300,000,000.00	-	Afya	Baadhi ya Vifaa vimenunuliwa
	UNICEF	HQ	Kuwezesha utekelezaji wa shughuli za chanjo ya Polio katika Vituo vya kutolea Huduma za Afya	98,700,000.00	98,700,000.00	-	Afya	Shughuli zimefanyika
	UNICEF	HQ	Kuwezesha uandaaji wa Mpango kabambe wa Idara ya Afya (CCHP) 2023/2024	38,000,500.00	38,000,500.00	-	Afya	Mpango kabambe umeandaliwa na umekamilika

	JHPIEGO	HQ	Kuwezesha utekelezaji wa shughuli za afya ya uzazi katika vituo vya kutolea Huduma za Afya	53,760,000.00	53,760,000.00	-	Afya	Shughuli zimefanyika
	ICAP	HQ	Kuwezesha utekelezaji wa shughuli za afya ya kupitia ICAP	50,803,960.00	50,803,960.00	-	Afya	Shughuli zimefanyika
	GLOBAL FUND	HQ	Kuwezesha ujenzi wa kichomea taka katika Hospitali ya Wilaya na shughuli za afya	69,853,123.62	69,853,123.62	-	Afya	Ujenzi umekamilika
	LISHE	HQ	Shughuli za Lishe	2,326,800.00	2,326,800.00	-	Afya	Shughuli zimefanyika
	GAVI	HQ	Kuwezesha utekelezaji wa shughuli za lishe	183,645,750.00	183,645,750.00		Afya	Shughuli zimefanyika
	GREEN AND SMART CITIES BURGET SURPORT	HQ	Kukamilisha shughuli za ujenzi katika jengo la Makao Makuu	500,000,000	500,000,000	-	Utawala	Mradi upo hatua ya ukamilishaji
	GREEN AND SMART CITIES BURGET SURPORT	HQ	Urekebishaji wa mgahawa uliopo karibu na jengo la Makao Makuu	35,000,000.00	28,108,919.00	6,891,081.00	Utawala	Hatua ya Maandalizi.
	GREEN AND SMART CITIES BURGET SURPORT	HQ	Ununuzi wa gari	170,000,000.00	0.00	170,000,000.00	Utawala	Halmashauri imeomba kibali kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu

	GREEN AND SMART CITIES BURGET SURPORT	HQ	Ununuzi wa Mabakuli 6 ya kuzolea taka na Dustbin.	100,000,000.00	100,000,000.00	-	Usafishaji na mazingira	Kontena zimenunuliwa
	GREEN AND SMART CITIES BURGET SURPORT	HQ	Ununuzi wa POS Mashine 50 za Ukusanyaji wa mapato	31,500,000.00	0.00	31,500,000.00	Fedha	Taratibu za manunuzi ya POS zinaendelea
	GREEN AND SMART CITIES BURGET SURPORT	HQ	Uandaaji wa maandiko miradi	30,000,000.00	30,000,000.00	-	Mipango na Uratibu	Jumla ya maandiko miradi manne yameandaliwa (mradi wa soko la Buswelu, Mwalo wa old Igombe, New Igombe na Soko la dagaa mwaloni)
	GREEN AND SMART CITIES BURGET SURPORT	HQ	Ununuzi wa kompyuta 1 ya Laptop	2,500,000.00	0.00	2,500,000.00	Tehama	Utekelezaji upo hatua ya manunuzi
	GREEN AND SMART CITIES BURGET SURPORT	HQ	Ununuzi wa kompyuta 1 ya mezani	2,000,000.00	0.00	2,000,000.00	Tehama	Utekelezaji upo hatua ya manunuzi
	GREEN AND SMART CITIES BURGET SURPORT		ununuzi wa printa 1 ya HP Laserjet	2,000,000.00	0.00	2,000,000.00	Tehama	Utekelezaji upo hatua ya manunuzi
	GREEN AND SMART CITIES BURGET SURPORT	HQ	Ununuzi wa projekta 1 ya Epson	2,000,000.00	0.00	2,000,000.00	Tehama	Utekelezaji upo hatua ya manunuzi

	GREEN AND SMART CITIES BURGET SURPORT	HQ	Ununuzi wa Canon photocopy machine 1	4,000,000.00	0.00	4,000,000.00	Tehama	Utekelezaji upo hatua ya manunuzi
	GREEN AND SMART CITIES BURGET SURPORT	HQ	Ununuzi wa drone 1 kwa picha za angani	5,000,000.00	0.00	5,000,000.00	Tehama	Utekelezaji upo hatua ya manunuzi
	Busket Fund	Vituo vya kutolea huduma za Afya zote	Vifaa tiba, Madawa	81,764,815.00	81,764,815.00	-	Afya	Vifaa tiba vimenunuliwa
	SERIKALI KUU (Elimu Bila Malipo sekondari)	Shule zote	Malipo ya Elimu bila malipo kwa Shule Sekondari	2,870,385,786.00	2,870,385,786.00	-	Elimu Sekondari	Fedha zote zimepokelewa
	SERIKALI KUU (Elimu Bila Malipo- Msingi)	Shule zote	Malipo ya Elimu bila malipo kwa Shule 76 za Msingi	1,200,688,494.10	1,200,688,494.10	-	Elimu Msingi	Fedha zote zimepokelewa
	SERIKALI KUU (Mfuko wa Jimbo)	HQ	Kuwezesha ununuzi wa saruji mifuko 1,231 kwa ajili ya mradi wa matofali ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari/Msingi Idadi ya tofali 39,585 zimefyatuliwa na kupelejkwa kwenye miradi ifuatayo:- 1.Wodi ya wazazi zahanati ya nyakato 6,000 2.Matundu 2 ya choo mwinuko	27,021,000.00	27,021,000.00	-	Elimu Sekondari/Msingi	Mifuko ya saruji 1,300 imenunuliwa.

			sekondari 1,574, 3.shule ya msingi nyamuge 3,500, 4.Madarasa 2 shule ya msingi kiloleli 2,000, 5.Wodi ya wazazi zahanati ya Luhanga 4,000, 6.Zahanati mpya Bwiru 2,500, 7.Zahanati ya nyambiti 3,000, 8.Ofisi ya serikali ya mtaa klimahewa A 700, 9.Ofisi za mitaa Lutongo na Iseni 1,600, 10.Ofisi ya serikali ya mtaa Lumala 3,500, 11.Kituo cha polisi mabatini 3,000, 12.Nyumba ya mtumishi 3,000, 13. parokia ya kiseke 1,000, 14.ofisi ys mtaa Nyasaka A 1,000, 15. Nyumba ya watumishi katibu UWT Ilemela 1,500					

	SERIKALI KUU (Mfuko wa Jimbo)	HQ	Kuwezesha ukarabati wa barabara za mitaa ambapo barabara zilizotengenezwa ni Buyombe – Zahanati ya Lukobe Kata ya Kahama, Barabara ya Zahanati ya Mihama Kata ya Kitangiri, barabara ya Kabuhoro – Kamachumu Kata ya Kirumba, barabara ya Nyasaka – Buswelu, barabara ya Bwiru Stand – Mnarani Sekondari Kata ya Pasiansi, na barabara ya Nyamwilekelwa Kata ya Mecco.	15,000,000.00	15,000,000.00	-	Ujenzi	Mradi umetekelezwa
	OWN SOURCE	HQ	Kuwezesha ununuzi wa POS Machine kwa ajli ya mfumo mpya wa TAUS	27,399,600.00	27,399,600.00	-	Fedha	POS zimenunuliwa
	OWN SOURCE	HQ	Kuwezesha ununuzi na ufungaji wa geti, vifaa vya umeme katika	6,515,000.00	6,515,000.00	-	Ujenzi	Kazi imekamilika

			Stendi ya Nyamhongolo					
	GREEN AND SMART CITIES BURGET SURPORT	Buzuruga, Kiloleli na Nyasaka	Ukarabati na matengenezo ya taa kando ya barabara ya buzuruga – kiloleli - nyasaka	100,000,000.00	100,000,000.00	-	Ujenzi	Matengenezo yanaendelea kufanyika
	JUMLA			**14,116,816,052.88**	**13,890,924,971.88**	**225,891,081.00**		
	KATA YA SANGABUYE							
	OWN SOURCE	SANGABUYE	Kuwezesha ujenzi wa ofisi ya serikali ya mtaa Nyamiswi	15,077,075.00	15,077,075.00	-	Utawala	Mradi umekamilika
	SERIKALI KUU (Mfuko wa Jimbo)	SANGABUYE	Kuwezesha Ukamilishaji wa jengo la malezi ya watoto wadogo Imalang'ombe	5,000,000.00	5,000,000.00	-	Ujenzi	Mradi umefikia hatua ya Upauaji
	OWN SOURCE	SANGABUYE	Kuwezesha kufungua barabara mradi wa viwanja Nyafula	58,873,000.00	58,873,000.00	-	Ujenzi	Mradi umekamilika
	OWN SOURCE	SANGABUYE	Kuwezesha Ukarabati wa matundu 6 ya vyoo Ihalalo shule ya Msingi	587,000.00	587,000.00	-	Elimu Msingi	Mradi umekamilika
	OWN SOURCE	SANGABUYE	Kuwezesha ukamilishaji wa boma, umeme, majisafi na	30,656,615.50	30,656,615.50	-	Afya	Miundombinu imekamilika

			majitaka, hospitali ya wilaya					
	OWN SOURCE	SANGABUYE	Kuwezesha ukamilishaji wa nyumba ya Mtumishi Kituo cha Afya Sangabuye	4,810,500.00	4,810,500.00	-	Afya	Mradi umekamilika
	TASAF	SANGABUYE	Kuwezesha ujenzi wa nyumba ya mtumishi zahanati ya Nyafula	47,080,960.21	0.00	47,080,960.21	Afya	Upo hatua ya maandalizi
	TASAF	SANGABUYE	Kuwezesha Ujenzi wa Jengo la Wagonjwa nje (OPD) Zahanati ya Nyafula	102,080,920.07	0.00	102,080,920.07	Afya	Upo hatua ya maandalizi
	S/KUU (Bweni)	SANGABUYE	Kuwezesha ukamilishaji wa bweni 1 Shule ya Sekondari Sangabuye	20,000,000.00	20,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Umekamilika
	TASAF	SANGABUYE	Kuwezesha Mradi wa Ufugaji wa mbuzi Kata ya Sangabuye	23,000,000.00	23,000,000.00	-	Kilimo, Mifugo na Uvuvi	Mbuzi zimenunuliwa na kugawiwa kwa vikundi
	JUMLA- SANGABUYE			**307,166,070.78**	**158,004,190.50**	**149,161,880.28**		
	KATA YA MECCO							
	MFUKO WA MHE. RAIS	MECCO	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 2 Shule ya Sekondari Nundu	40,000,000.00	40,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika

	OWN SOURCE	MECCO	Kuwezesha ujenzi wa Ofisi ya Kata	5,000,000.00	5,000,000.00	-	Utawala	Mradi unaendelea
	JUMLA -MECCO			**45,000,000.00**	**45,000,000.00**	**-**		
	KATA YA BUZURUGA							
	SEQUIP	BUZURUGA	Kuwezesha ujenzi wa Nyumba za Walimu Shule ya Sekondari Buzuruga	100,000,000.00	0.00	100,000,000.00	Elimu Sekondari	Hatua ya maandalizi
	OWN SOURCE	BUZURUGA	Kuwezesha ujenzi wa chumba cha ICT Shule ya Sekondari Buzuruga	30,000,000.00	30,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Chumba cha ICT kimekamilika
	OWN SOURCE	BUZURUGA	Kuwezesha ukamilishaji wa choo na Maabara Shule ya Sekondari Buzuruga	30,000,000.00	30,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika
	MFUKO WA MHE. RAIS	BUZURUGA	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 14 Shule ya Sekondari Buzuruga	280,000,000.00	280,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika
	OWN SOURCE	BUZURUGA	Kuwezesha ujenzi wa wodi ya akina mama katika kituo cha afya Buzuruga	199,032,000.00	199,032,000.00	-	Afya	Mradi umekamilika
	OWN SOURCE	BUZURUGA	Kuwezesha ukamilishaji wa Ofisi ya Serikali ya Mtaa Buzuruga Kaskazini	15,077,075.00	15,077,075.00	-	Utawala	Mradi umekamilika
	JUMLA -BUZURUGA			**654,109,075.00**	**554,109,075.00**	**100,000,000.00**		
	KATA YA NYAMHONGOLO							

	OWN SOURCE	NYAMHONGOLO	Ujenzi wa Kibanda stendi ya Nyamhongolo	1,706,500.00	1,706,500.00	-	Biashara, Viwanda na Uwekezaji	Mradi unaendelea
	OWN SOURCE	NYAMHONGOLO	Kuwezesha ujenzi wa nyumba ya mwalimu NYAMHONGOLO shule ya Msingi	16,000,000.00	15,985,700.00	14,300.00	Elimu Msingi	Mradi upo hatua ya umaliziaji
	LANES	NYAMHONGOLO	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 2 ya awali ya mfano Nyamadoke S/M	55,824,000.00	55,824,000.00	-	Elimu Msingi	Ujenzi umekamilika
	BOOST	NYAMHONGOLO	Kuwezesha ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa Shule ya Msingi Nyamadoke	100,000,000.00	100,000,000.00	-	Elimu Msingi	Mradi umekamilika
	BOOST	NYAMHONGOLO	Kuwezesha ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa Shule ya Msingi Nyamhongolo	100,000,000.00	100,000,000.00	-	Elimu Msingi	Mradi umekamilika
	BOOST	NYAMHONGOLO	Kuwezesha ujenzi wa Matundu 3 ya vyoo Shule ya Msingi Nyamadoke	6,300,000.00	6,300,000.00	-	Elimu Msingi	Mradi umekamilika
	BOOST	NYAMHONGOLO	Kuwezesha ujenzi wa Matundu 3 ya vyoo Shule ya Msingi Nyamhongolo	6,300,000.00	6,300,000.00	-	Elimu Msingi	Mradi umekamilika
	OWN SOURCE	NYAMHONGOLO	Kuwezesha ujenzi wa jengo la RCH zahanati ya	8,853,275.00	8,815,500.00	37,775.00	Afya	Ujenzi umekamilika

			Nyamhongolo					
	GREEN AND SMART CITIES BURGET SURPORT	NYAMHONGOLO	Kuunganisha mfumo wa ukusanyaji mapato (GOTHOMIS) Kituo cha Afya Nyamadoke	16,000,000.00	16,000,000.00	-	Afya	Vifaa vimenunuliwa na Maandalizi ya uunganishaji mfumo yanaendelea
	MFUKO WA MHE. RAIS	NYAMHONGOLO	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 7 Shule ya Sekondari Ibinza	140,000,000.00	140,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika
	MFUKO WA MHE. RAIS	NYAMHONGOLO	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 6 Shule ya Sekondari Nyamhongolo	120,000,000.00	120,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika
	TASAF	NYAMHONGOLO	Kuwezesha Mradi wa Ufugaji wa mbuzi Kata ya Sangabuye, na Nyamhongolo	21,199,627.59	21,199,627.59	-	Kilimo, Mifugo na Uvuvi	Mbuzi zimenunuliwa na kugawiwa kwa vikundi vimegawiwa
	SERIKALI KUU (Mfuko wa Jimbo)	NYAMHONGOLO	Kuwezesha Maombi ya mifuko 100 ya saruji kwa ajili ya kuinua boma kituo cha Polisi Nyamhongolo	2,300,000.00	2,300,000.00	-	Utawala	Mradi upo hatua ya boma
	JUMLA -NYAMHONGOLO			**594,483,402.59**	**594,431,327.59**	**52,075.00**		
	KATA YA IBUNGILO							
	OWN SOURCE	IBUNGILO	Kuwezesha ujenzi wa ukuta wa mawe Shule ya sekondari Ibungilo	3,820,000.00	3,820,000.00	-	Elimu Sekondari	Ukuta umejengwa

	MFUKO WA MHE. RAIS	IBUNGILO	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 4 Shule ya Sekondari Ibungilo	80,000,000.00	80,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika
	EP4R	IBUNGILO	Kuwezesha ujenzi wa nyumba ya watumishi 2 in 1 Shule ya msingi Hekima	50,000,000.00	50,000,000.00	-	Elimu Msingi	Mradi umekamilika
	OWN SOURCE	IBUNGILO	Kuwezesha ukamilishaji wa darasa shule ya msingi Kiloleli	12,500,000.00	12,500,000.00	-	Elimu Msingi	Mradi umekamilika
	OWN SOURCE	IBUNGILO	Kuwezesha Ukarabati wa matundu 7 ya vyoo Ihalalo shule ya Msingi	3,929,000.00	3,929,000.00	-	Elimu Msingi	Mradi upo hatua ya umaliziaji
	OWN SOURCE	IBUNGILO	Kuwezesha ujenzi wa matundu 10 ya vyoo shule ya msingi Ibungilo	11,089,000.00	11,089,000.00	-	Elimu Msingi	Mradi upo hatua ya umaliziaji
	OWN SOURCE	IBUNGILO	Kuwezesha ukarabati wa soko la Kiloleli	4,406,000.00	4,406,000.00	-	Biashara, Viwanda na Uwekezaji	Marekebisho yamefanyika
	JUMLA - IBUNGILO			**165,744,000.00**	**165,744,000.00**	**-**		
	KATA YA KIRUMBA							
	OWN SOURCE	KIRUMBA	Kuwezesha Matengenezo ya mzani Mwaloni	14,194,928.00	14,194,928.00	-	Ujenzi	Matengenezo yamefanyika
	OWN SOURCE	KIRUMBA	Kuwezesha ujenzi wa barabara ya Kazamoyo	7,010,000.00	7,010,000.00	-	Ujenzi	Mradi unaendelea

	OWN SOURCE	KIRUMBA	Kuwezesha matengenezo ya Jenereta ya soko la Kimataifa la Dagaa Mwaloni Kirumba	990,000.00	990,000.00	-	Ujenzi	Matengenezo yamefanyika
	TASAF	KIRUMBA	Kuwezesha ujenzi wa barabara za mawe katika kata ya Kirumba	215,376,907.32	48,994,000.00	166,382,907.32	Ujenzi	Mradi unaendelea
	OWN SOURCE	KIRUMBA	Kuwezesha uwekaji wa mradi wa umeme na maji katika soko la muda la Magomeni	8,430,289.33	8,430,289.33	-	Biashara, Viwanda na Uwekezaji	Mradi umekamilika
	OWN SOURCE	KIRUMBA	Kuwezesha ununuzi wa Computer Desktop kwaajili ya kutolea huduma ya kupima uzito wa magari Kirumba Mwaloni	4,367,184.00	4,367,184.00	-	Tehama	Vifaa vimenunuliwa
	MFUKO WA MHE. RAIS	KIRUMBA	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 5 Shule ya Sekondari Kabuhoro	100,000,000.00	100,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika
	SERIKALI KUU (Maabara)	KIRUMBA	Kuwezesha ukamilishaji wa maabara 1 shule ya Sekondari Kirumba	30,000,000.00	30,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Umekamilika
	SERIKALI KUU (Maabara)	KIRUMBA	Kuwezesha ukamilishaji wa maabara 1 shule ya Sekondari	30,000,000.00	30,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Umekamilika

			Kabuhoro					
	MFUKO WA MHE. RAIS	KIRUMBA	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 1 Shule ya Sekondari Kirumba	20,000,000.00	20,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika
	JUMLA - KIRUMBA			**430,369,308.65**	**263,986,401.33**	**166,382,907.32**		
	KATA YA KAYENZE							
	MFUKO WA MHE. RAIS	KAYENZE	Kuweshesha ujenzi wa madarasa 2 Shule ya Sekondari Kayenze	40,000,000.00	40,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika
	OWN SOURCE	KAYENZE	Kuwezesha ukamilishaji wa matundu ya Vyoo katika eneo la uanikaji dagaa Mwalo wa KAYENZE	4,311,350.00	4,311,350.00	-	Ujenzi	Mradi unaendelea
	SERIKALI KUU (Mfuko wa Jimbo)	KAYENZE	Kuwezesha Ukamilshaji wa Ofisi ya Mtaa wa Iponyabugali	2,500,000.00	2,500,000.00	-	Utawala	Mradi umekamilika
	SERIKALI KUU (Mfuko wa Jimbo)	KAYENZE	Ukarabati wa Nyumba ya Mwalimu S/M Kayenze	3,000,000.00	3,000,000.00	-	Elimu Msingi	Ukarabati Unaendelea
	JUMLA - KAYENZE			**49,811,350.00**	**49,811,350.00**	**-**		
	KATA YA KITANGIRI							
	MFUKO WA MHE. RAIS	KITANGIRI	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 1 Shule ya Sekondari	20,000,000.00	20,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika

			Mwinuko					
	OWN SOURCE	KITANGIRI	Kuwezesha ujenzi wa choo matundu 6 katika soko la Kitangiri	10,826,928.00	10,826,928.00	-	Ujenzi	Mradi unaendelea
	SERIKALI KUU (Mfuko wa Jimbo)	KITANGIRI	Kuwezesha Ujenzi wa Nyumba ya Mtumishi Zahanati ya Kitangiri Kati	5,000,000.00	-	5,000,000.00	Afya	Msingi umekamilika
	TASAF	KITANGIRI	Kuwezesha ujenzi wa Zahanati kata ya Mihama	92,779,762.49	92,779,762.49	-	Afya	Umekamilika
	TASAF	KITANGIRI	Kuwezesha ujenzi wa nyumba ya mtumishi Jengo la ukunga na vyoo matundu 4- Zahanati ya Mihama	94,586,779.06	94,586,779.06	-	Afya	Umekamilika
	JUMLA- KITANGIRI			**223,193,469.55**	**218,193,469.55**	**5,000,000.00**		
	KATA YA PASIANSI							
	OWN SOURCE	PASIANSI	Kuwezesha utengenezaji wa vitanda shule ya sekondari ya wavulana Bwiru	7,500,000.00	7,500,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika
	OWN SOURCE	PASIANSI	Kuwezesha ukamilishaji wa bweni la shule ya sekondari ya wavulana Bwiru	58,000,000.00	58,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika

	MFUKO WA MHE. RAIS	PASIANSI	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 5 Shule ya Sekondari Kitangiri	100,000,000.00	100,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika
	SERIKALI KUU	PASIANSI	Ujenzi wa madarasa 3 Shule ya Sekondari Bwiru Wasichana	75,000,000.00	70,845,883.00	4,154,117.00	Elimu Sekondari	Hatua ya kupaka rangi
	SERIKALI KUU	PASIANSI	Ujenzi wa bweni 1 Shule ya Sekondari Bwiru Wasichana	130,000,000.00	128,669,245.00	1,330,755.00	Elimu Sekondari	Hatua ya kupaka rangi
	SERIKALI KUU	PASIANSI	Ujenzi wa matundu 5 ya vyoo Shule ya Sekondari Bwiru Wasichana	10,500,000.00	9,660,000.00	840,000.00	Elimu Sekondari	Hatua ya ukamilishaji
	EP4R	PASIANSI	Kuwezesha ujenzi wa maabara ya Sayansi katika Shule ya Sekondari Bwiru Wasichana	50,000,000.00	50,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika
	OWN SOURCE	PASIANSI	Kuwezesha ujenzi wa Zahanati ya Bwiru	5,000,000.00	5,000,000.00	-	Afya	Mradi unaendelea
	OWN SOURCE	PASIANSI	Kuwezesha matengenezo ya barabara ya mtaa Bwiru ziwani	7,000,000.00	7,000,000.00	-	Ujenzi	Mradi umekamilika
	JUMLA - PASIANSI			**443,000,000.00**	**436,675,128.00**	**6,324,872.00**		
	KATA YA SHIBULA							

	OWN SOURCE	SHIBULA	Kuwezesha Malipo kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya madarasa 7 na ofisi 2 katika shule ya msingi ilioko kata ya Shibula	84,257,000.00	84,257,000.00	-	Elimu Msingi	Mradi umekamilika
	OWN SOURCE	SHIBULA	Kuwezesha ujenzi na ukamilishaji wa matundu 10 ya choo na ofisi 2 Shule ya Msingi Shibula	22,926,375.00	22,926,375.00	-	Elimu Msingi	Mradi unaendelea
	SERIKALI KUU (Mfuko wa Jimbo)	SHIBULA	Kuwezesha Utengenezaji wa madawati 50 ya Shule za Msingi kupunguza idadi ya watoto wanaokaa chini	3,500,000.00	3,500,000.00	-	Elimu Msingi	Madawati yamekamilika
	SERIKALI KUU (Mfuko wa Jimbo)	SHIBULA	Kuwezesha Uwekaji umeme shule msingi Shibula	320,000.00	-	320,000.00	Elimu Msingi	Mradi unasubiri uhakiki kutoka TANESCO
	BOOST	SHIBULA	Kuwezesha ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa Shule ya Msingi Nyamwilolelwa	100,000,000.00	100,000,000.00	-	Elimu Msingi	Mradi umekamilika
	BOOST	SHIBULA	Kuwezesha ujenzi wa Matundu 3 ya vyoo Shule ya	6,300,000.00	6,300,000.00	-	Elimu Msingi	Mradi umekamilika

			Msingi Nyamwililelwa					
	MFUKO WA MHE. RAIS	SHIBULA	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 3 Shule ya Sekondari Semba	60,000,000.00	60,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika
	MFUKO WA MHE. RAIS	SHIBULA	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 9 Shule ya Sekondari Shibula	180,000,000.00	180,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika
	OWN SOURCE	SHIBULA	Kuwezesha ujenzi wa jengo la kujifungulia Zahanati ya Nyamwililelwa	26,812,000.00	26,812,000.00	-	Afya	Mradi umekamilika
	OWN SOURCE	SHIBULA	Kuwezesha ujenzi wa barabara shule ya sekondari Semba kata ya Shibula	3,092,000.00	3,092,000.00	-	Ujenzi	Mradi unaendelea
	JUMLA- SHIBULA			**487,207,375.00**	**486,887,375.00**	**320,000.00**		
	KATA YA KAHAMA							
	OWN SOURCE	KAHAMA	Kuwezesha Ununuzi wa eneo la ujenzi wa shule ya msingi Kata ya Kahama	2,000,000.00	2,000,000.00	-	Elimu Msingi	Eneo limenunuliwa
	OWN SOURCE	KAHAMA	Malipo kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya madarasa 5 katika shule ya msingi ilioko katika kata ya	71,200,000.00	71,200,000.00	-	Elimu Msingi	Mradi umekamilika

			Kahama					
	OWN SOURCE	KAHAMA	Kuwezesha utengenezaji wa madawati ya Shule ya msingi iliyopo Kata ya Kahama	29,194,000.00	29,194,000.00	-	Elimu Msingi	Madawati yametengenezwa
	OWN SOURCE	KAHAMA	Kuwezesha ujenzi wa matundu 20 ya vyoo shule ya msingi Lukobe	20,000,000.00	20,000,000.00	-	Elimu Msingi	Mradi umekamilika
	BOOST	KAHAMA	Kuwezesha ujenzi wa Shule Mpya yenye Mikondo 2 Shule ya Msingi Kahama	540,300,000.00	470,761,532.61	69,538,467.39	Elimu Msingi	Mradi uko hatua ya ukamilishaji
	MFUKO WA MHE. RAIS	KAHAMA	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 4 Shule ya Sekondari Lukobe	80,000,000.00	80,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika
	SERIKALI KUU (Mfuko wa Jimbo)	KAHAMA	Kuwezesha Umaliziaji wa Jengo la maabara Zahanati ya Kata ya Kahama	5,580,000.00	3,480,000.00	2,100,000.00	Afya	Boma limekamilika, mradi unaendelea
	JUMLA - KAHAMA			**748,274,000.00**	**676,635,532.61**	**71,638,467.39**		
	KATA YA NYAKATO							
	OWN SOURCE	NYAKATO	Kuwezesha Malipo kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo 15 katika shule ya msingi iliyoko kata ya Nyakato	20,000,000.00	20,000,000.00	-	Elimu Msingi	Mradi umekamilika

	OWN SOURCE	NYAKATO	Kuwezesha ujenzi wa vyumba 5 vya madarasa shule ya msingi Kangaye	54,000,000.00	54,000,000.00	-	Elimu Msingi	Mradi umekamilika
	SERIKALI KUU (Mfuko wa Jimbo)	NYAKATO	Kuwezesha Uwekaji Umeme shule mpya Kangae Shule ya Msingi	320,000.00	320,000.00	-	Elimu Msingi	Mradi umekamilika na umeme unawaka
	SERIKALI KUU (Mfuko wa Jimbo)	NYAKATO	Kuwezesha Mradi wa Maji mtaa wa Kangae	4,000,000.00	4,000,000.00	-	Maji	Mradi umekamilika na maji yanatoka
	MFUKO WA MHE. RAIS	NYAKATO	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 6 Shule ya Sekondari Kangaye	120,000,000.00	120,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika
	JUMLA NYAKATO			**198,320,000.00**	**198,320,000.00**	**-**		
	KATA YA BUSWELU							
	OWN SOURCE	BUSWELU	Ukarabati wa nyumba ya mwalimu Buwelu	4,000,000.00	4,000,000.00	-	Elimu Msingi	Ukarabati umefanyika
	OWN SOURCE	BUSWELU	Kuwezesha ujenzi wa Bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalum Buswelu S/M	3,619,000.00	3,619,000.00	-	Elimu Msingi	Ujenzi upo hatua ya lenta
	OWN SOURCE	BUSWELU	Kuwezesha ukamilishaji wa vyumba 2 vya madarasa Bujingwa S/M	20,440,000.00	20,440,000.00	-	Elimu Msingi	Ujenzi upo hatua ya kupaka rangi na vigae
	LANES	BUSWELU	Kuwezesha ujenzi wa Bweni la wanafunzi wenye	100,000,000.00	100,000,000.00	-	Elimu Msingi	Upo hatua ya umaliziaji

			mahitaji maalum					
	SERIKALI KUU (Mfuko wa Jimbo)	BUSWELU	Kuwezesha ujenzi wa matundu manne ya vyoo shule ya Msingi Buhyila ambayo ni shule mpya	4,400,000.00	4,400,000.00	-	Elimu Msingi	Ujenzi upo hatua ya lenta
	BOOST	BUSWELU	Kuwezesha ujenzi wa Shule Mpya yenye Mikondo 2 Shule ya Msingi Buswelu	540,300,000.00	466,580,008.31	73,719,991.69	Elimu Msingi	Mradi uko hatua ya ukamilishaji
	SERIKALI KUU (Mfuko wa Jimbo)	BUSWELU	Kuwezesha Uvutaji wa Maji Shule ya Sekondari Bujingwa	500,000.00	500,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika na maji yanatoka
	OWN SOURCE	BUSWELU	Kuwezesha ujenzi wa mashimo ya vyoo katika shule ya sekondari Bujingwa	4,821,060.00	4,821,060.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika
	MFUKO WA MHE. RAIS	BUSWELU	Kuwezesha ujenzi wa vyumba vya madarasa 8 Shule ya Sekondari Bujingwa	160,000,000.00	160,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika
	MFUKO WA MHE. RAIS	BUSWELU	Kuwezesha ujenzi wa vyumba vya madarasa 8 Shule ya Sekondari Buswelu	160,000,000.00	160,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika

	OWN SOURCE	BUSWELU	Kuwezesha utengenezaji wa Bustani ya Lishe nauwekaji wa uzio katika bustani ya lishe Buswelu S/M	6,360,000.00	6,360,000.00	-	Afya	Bustani imetengenezwa
	JUMLA -BUSWELU			**1,004,440,060.00**	**930,720,068.31**	**73,719,991.69**		
	KATA YA NYASAKA							
	OWN SOURCE	NYASAKA	Kuwezesha malipo ya pango la ardhi kiwanja cha shule ya msingi Kata ya Nyasaka	4,523,650.00	4,523,650.00	-	Elimu Msingi	Malipo yamefanyika
	OWN SOURCE	NYASAKA	Kuwezesha ukamilishaji wa jengo la Mama na Mtoto zahanati ya Chamwenda	33,853,200.00	-	33,853,200.00	Afya	Mradi upo hatua ya manunuzi
	JUMLA NYASAKA			**38,376,850.00**	**4,523,650.00**	**33,853,200.00**		
	KATA YA KISEKE							
	OWN SOURCE	KISEKE	Kuwezesha ukamilishaji wa darasa 1 na ofisi ya M/Mkuu S/M Kiseke	12,500,000.00	12,500,000.00	-	Elimu Msingi	Mradi upo hatua ya umaliziaji
	MFUKO WA MHE. RAIS	KISEKE	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 6 Shule ya Sekondari Angelina Mabula	120,000,000.00	120,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika
	SERIKALI KUU (Maabara)	KISEKE	Kuwezesha ukamilishaji wa maabara 1 shule ya Sekondari Angelina Mabula	30,000,000.00	30,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Umekamilika

	SEQUIP	KISEKE	Kuwezesha Ujenzi wa Shule Mpya ya Sekondari ya Kata	584,280,028.00	0.00	584,280,028.00	Elimu Sekondari	Hatua ya maandalizi
	JUMLA - KISEKE			**746,780,028.00**	**162,500,000.00**	**584,280,028.00**		
	KATA YA KAWEKAMO							
	MFUKO WA MHE. RAIS	KAWEKAMO	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 3 Shule ya Sekondari Kilimani	60,000,000.00	60,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika
	OWN SOURCE	KAWEKAMO	Kuwezesha ukamilishaji wa Zahanati kata ya Kawekamo	73,611,750.00	73,611,750.00	-	Afya	Mradi upo hatua ya umaliziaji
	JUMLA- KAWEKAMO			**133,611,750.00**	**133,611,750.00**	**-**		
	KATA YA BUGOGWA							
	OWN SOURCE	BUGOGWA	Kuwezesha ununuzi wa vifaa vya maji, umeme na saruji kwaajili ya ukarabati wa chumba cha X- ray Kituo cha Afya Karume	3,939,057.44	3,939,057.44	-	Afya	Vifaa vimenunuliwa
	EP4R	BUGOGWA	Kuwezesha ujenzi wa nymba ya watumishi 2 in 1 Shule ya msingi Isanzu	50,000,000.00	50,000,000.00	-	Elimu Msingi	Mradi umekamilika
	BOOST	BUGOGWA	Kuwezesha ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa Shule ya Msingi Igombe	100,000,000.00	100,000,000.00	-	Elimu Msingi	Mradi umekamilika

	BOOST	BUGOGWA	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 2 ya mfano Elimu ya Awali Shule ya Msingi Chasubi	69,100,000.00	69,100,000.00	-	Elimu Msingi	Mradi umekamilika
	BOOST	BUGOGWA	Kuwezesha ujenzi wa Matundu 3 ya vyoo Shule ya Msingi Igombe	6,300,000.00	6,300,000.00	-	Elimu Msingi	Mradi umekamilika
	MFUKO WA MHE. RAIS	BUGOGWA	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 10 Shule ya Sekondari Bugogwa	200,000,000.00	200,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika
	MFUKO WA MHE. RAIS	BUGOGWA	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 1 Shule ya Sekondari Igogwe	20,000,000.00	20,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika
	SERIKALI KUU (Maabara)	BUGOGWA	Kuwezesha ukamilishaji wa maabara 1 shule ya Sekondari Kisundi	30,000,000.00	30,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Umekamilika
	TASAF	BUGOGWA	Kuwezesha ujenzi wa nyumba ya mwalimu 2 in 1 Shule ya Sekondari Igogwe	93,783,399.95	0.00	93,783,399.95	Elimu Sekondari	Upo hatua ya maandalizi
	TASAF	BUGOGWA	Kuwezesha ujenzi wa Maktaba Shule ya Sekondari Igogwe	102,354,028.00	0.00	102,354,028.00	Elimu Sekondari	Upo hatua ya maandalizi
	TASAF	BUGOGWA	Kuwezesha ujenzi wa Hosteli ya wavulana 80 Shule	150,741,852.29	0.00	150,741,852.29	Elimu Sekondari	Upo hatua ya maandalizi

			ya Sekondari Igogwe					
	TASAF	BUGOGWA	Kuwezesha ujenzi wa Maabara ya Sayansi ya pili Shule ya Sekondari Igogwe	65,190,698.62	65,190,698.62	-	Elimu Sekondari	Umekamilika
	TASAF	BUGOGWA	Kuwezesha ujenzi wa Hosteli ya Wasichana 80 Igogwe Sekondari	142,630,366.16	142,630,366.16	-	Elimu Sekondari	Umekamilika
	MFUKO WA MHE. RAIS	BUGOGWA	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 2 Shule ya Sekondari Kisundi	40,000,000.00	40,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika
	SERIKALI KUU (Mfuko wa Jimbo)	BUGOGWA	Kuwezesha uwekaji umeme Igogwe Sekondari	320,000.00	-	320,000.00	Elimu Sekondari	Mmradi unasubiri nguzo toka TANESCO
	JUMLA- BUGOGWA			**1,074,359,402.46**	**727,160,122.22**	**347,199,280.24**		
	KATA YA ILEMELA							
	MFUKO WA MHE. RAIS	ILEMELA	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 2 Shule ya Sekondari Lumala	40,000,000.00	40,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika
	SERIKALI KUU (Mfuko wa Jimbo)	ILEMELA	Ununuzi wa pikipiki mbili za kikundi cha sanaa na umoja wa bodaboda Ilemela.	5,000,000.00	5,000,000.00	-	Utawala	Manunuzi yamefanyika GPSA hatua ya malipo

								imekamilika
	JUMLA- ILEMELA			**45,000,000.00**	**45,000,000.00**	**-**		
	KATA YA NYAMANORO							
	MFUKO WA MHE. RAIS	NYAMANORO	Kuwezesha ujenzi wa madarasa 1 Shule ya Sekondari Nyamanoro	20,000,000.00	20,000,000.00	-	Elimu Sekondari	Mradi umekamilika
	JUMLA NYAMANORO			**20,000,000.00**	**20,000,000.00**	**-**		
	JUMLA KUU KWENYE MIRADI KWA MWAKA 2022/2023			**21,526,062,194.91**	**19,762,238,411.99**	**1,763,823,782.92**		